



BUSEGA DEVELOPMENT COMMUNITY
JUMUIYA YA MAENDELEO YA WANABUSEGA

DATE
Tarehe
07/09/2014

REFERENCE
Kumbukumbu
BUDECO/HQ/GF/006

**TAMKO LA WANABUSEGA WAISHIO DAR ES LAAM KULAANI KITENDO CHA UBAKAJI
ALICHOFANYIWA MWALIMU WA SHULE YA SEKONDARI KISHAMAPANDA KATIKA
WILAYA YA BUSEGA TAREHE 23/08/2014.**

Ndg wanahabari: Tumewaita leo hii ili kuzungumzia na kulaani kitendo cha kinyama na cha aibu alichofanyiwa mwalimu wa shule ya Sekondari Kishamapanda iliyoko Wilaya ya Busega, Mkoa wa Simiyu.

BUDECO NI NANI?

BUDECO ni Jumuiya ya Maendeleo ya Wanabusega (Busega Development Community). Hii ni Asasi isiyo ya Kiserikali, Kidini, Kisiasa wala Kikabila inayowaunganisha Wanabusega wote katika kuchangia na kuhamasisha shughuli mbali mbali za Maendeleo ya Kijamii katika Wilaya ya Busega. BUDECO ni Asasi iliyoundwa kwa mujibu wa sheria na kusajiliwa chini ya sheria ya Vyama vya Kijamii (**CAP. 337 R.E.2002**) na kupewa cheti cha usajili Na. S.A. 19055, Oktoba 2013.

JINSI ILIVYOKUWA SIKU YA TUKIO.

Ilikuwa mnamo saa 8 usiku tarehe 23/08/2014, kundi la watu wasiofahamika walivamia nyumbani kwa **Mwl Samwel M. Mkumbo** (ambako mwalimu aliye bakwa amepanga) wakiwa na mapanga, mashoka na zana zingine. Majambazi hao walimteka **Mwl Mkumbo** na kumpora fedha kiasi cha takribani sh. Millioni 18.

Baada ya uporaji huo, majambazi hao walivamia nyumba ambayo **Mwalimu wa shule ya sekondari Kishamapanda** amepanga, walivunja mlango na kuingia ndani.

Mwalimu huyo aliamrisha ajisalimishe sebuleni la sivyo wakiingia chumbani watamuua. Haikuchukua muda majambazi hao walivunja mlango wa chumbani na kuanza kumpiga huku wakimwamrisha awape hela. Mwalimu huyo alikuwa na sh. 50,000/- tu, ambazo aliwaambia wachukue kwenye pochi iliyokuwa mezani. Majambazi hao walichukua fedha hizo pamoja na simu yake ya mkononi. Baada ya hapo waliamua kumbaka kwa mande (zamu).

Baada ya wahalifu hao kutimiza unyama huo waliondoka na ndipo mwalimu huyo alipiga kelele za kuomba msaada kwa majirani. Majirani walimsaidia kumpeleka kituo cha polisi na kisha hospitalini.

Postal Address
P.O. BOX 31201,
DAR ES SALAAM
TANZANIA.

Telephone/Mobile
+255 784 590 831
+255 762 835 555

Website: www.budeco.co.tz
E-mail: uongozi@budeco.co.tz



BUSEGA DEVELOPMENTCOMMUNITY
JUMUIYA YA MAENDELEO YA WANABUSEGA

DATE
Tarehe
07/09/2014

REFERENCE
Kumbukumbu
BUDECO/HQ/GF/006

Ndugu Wanahabari: Sisi Jumuiya ya Wanabusega tumesikitishwa sana na matukio waliyofanyiwa walimu hao, hivyo;

- Tunalaani kwa nguvu zote tukio la kubakwa kwa mwalimu huyo, kwani ni kitendo cha kinyama kisichovumilika katika jamii iliyostaarabika ambalo pia ni udhalilishaji wa utu wa mtu.
- Tunalaani vikali tukio la kubakwa kwa mwalimu huyo, kwani ni tendo la uuaji ambalo limetokea wakati nchi yetu na dunia kwa ujumla zikiwa katika mapambano makali dhidi ya maambukizo ya VVU/UKIMWI. Tunamwombea kwa mwenyezi MUNGU amwepushie mbali na maradhi hayo.
- Tunalaani kwa nguvu zote tukio la kubakwa kwa mwalimu huyo, kwani linalrudisha nyuma jitihada za serikali na jamii nzima ya Wanabusega katika maendeleo ya elimu ikizingatiwa kuwa wilaya yetu ni moja kati ya Wilaya mpya hapa nchini.
- Tunalaani kwa nguvu zote tukio la kubakwa kwa mwalimu huyo, kwani zitawaogopesha walimu na watumishi wengine wa Umma kufanya kazi katika Wilaya ya Busega.
- Pia tunalaani tukio la uporaji wa mamilioni ya hela aliyofanyiwa mwalimu Mkumbo, kwani yanarudisha nyuma jitihada za wananchi katika kujiletea maendeleo yao.

Jumuiya ya Wanabusega inalaani vikali vitendo hivyo vyote vilivyofanyiwa na waovu hao. Tunaomba wahusika wote wa matukio hayo wasakwe, wakamatwe na wafikishwe mbele ya sheria ili sheria ichukue mkondo wake.

Vile vile tunalaani vikali matendo ya ujambazi na ubakaji wanayofanyiwa wanawake na watoto popote nchini. Tunaiomba Serikali na vyombo vyake vya dola kukomesha vitendo hivi ambavyo vimezidi kushamiri katika nchi yetu katika miaka ya hivi karibuni.

Ahsante.

(imesainiwa)

Maselle J. Ginhu

Mwenyekiti - BUDECO

Postal Address
P.O. BOX 31201,
DAR ES SALAAM
TANZANIA.

Telephone/Mobile
+255 784 590 831
+255 762 835 555

Website: www.budeco.co.tz
E-mail: uongozi@budeco.co.tz